




Hapo zamani,  
wanyama hawakuwa  
na miguu.




Maguru alikuwa  
amewapatia miguu  
watu pekee.



Maguru aliamua  
kumpatia kila mnyama  
miguu.




Wanyama walitaka  
miguu ili watembee na  
kukimbia.




Ilikuwa vigumu kwao  
kutambaa.



Siku ilifika. Wanyama  
tofauti walitambaa  
kwenda kwa Maguru.



Maguru aliwapatia  
wanyama na ndege  
miguu.



Baadhi ya wanyama  
walicheza. Wengine  
walianguka chini.



Walisema,  
"Hatutatambaa tena."



Jongoo alikuwa wa  
mwisho kwenye  
mstari.



Maguru alimpatia  
miguu yote iliyokuwa  
imabaki.



Jongoo alisema kwa  
furaha, "Nitatembea  
haraka kuwaliko  
wengine."



Baadaye, Nyoka alifika.  
Alimsihi Maguru,  
“Tafadhali, nipe  
miguu.”



Nyoka alimwambia  
Maguru, "Nililala  
kupita kiasi."



Maguru hakupata  
miguu yoyote ya  
kumpatia Nyoka.



Tangu siku hiyo,  
Nyoka anasubiri  
kupata miguu.